

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

04/04/2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA ATOA AHADI YA KUWAPATIA MILIONI 10 CHAMA CHA WAJANE NA KUWAJENGEA JENGO LA KISASA LA MAKAO MAKUU.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda ameahidi kuwapatia shilingi milioni 10 chama cha wajane Tanzania kama sehemu ya sadaka yake ya Jumapili ili kuhakikisha wajane wanapata ofisi ya kudumu ya kushughulikia mambo yao.

Kutokana na hilo RC Makonda amewaagiza Wakuu wa Wilaya kutafuta eneo maalumu ambalo litafaa kujenga ofisi za kisasa za Makao Makuu ya Chama cha wajane.

Hatua ya RC Makonda kutoa ahadi hiyo ni baada ya kusikia kilio cha wajane ambao wameeleza kuwa wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ofisi ya kudumu jambo linalowalazimu kufanya shughuli zao katika jengo la Kukodi na wakati mwingine wanakosa fedha za kulipia kodi ya pango.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM